

SIKU YA TAKWIMU AFRIKA 2020: SHINDANO LA WAANDISHI BORA WA HABARI ZA KITAKWIMU

Ofisi ya Taifa ya Takwimu imeandaa shindano la Waandishi Bora wa habari za kitakwimu kama sehemu ya Maadhimisho ya Siku ya Takwimu Afrika 2020.

Shindano hili linahusisha waandishi wa habari walioajiriwa au wakujitegemea kutoka kwenye Taasisi /Chombo cha Habari.

Makala hizo ziwe zimeshapishwa kwenye gazeti au mtandaoni kuanzia Disemba, 2019 mpaka tarehe 10 Novemba, 2020.

SIFA ZA MAKALA/HABARI

1. Makala/Habari husika iwe ya uchambuzi wa kina wa mada inayochambua kilichomo kwenye takwimu na iwe kwenye lugha rahisi inayoeleweka;
2. Lugha ya picha inatakiwa iwe rahisi wakati wa kuelezea maudhui ya kilichowasilishwa;
3. Inapaswa kujumuisha vyanzo vya kuaminika vya habari ili kuongeza thamani/ladha ya habari inayoelezea takwimu hizo;
4. Makala/Habari iwe yenye Ushahidi wa Takwimu ambazo zimeandaliwa na mwandishi kwa kuchambua na kuhoji ripoti rasmi ya takwimu (Statistical report) ili kupata taarifa au ujumbe zaidi uliokusudiwa katika jamii.
5. Makala/ Habari inapaswa itoe takwimu zenye malengo ya kibinadamu/kumgusa mtu au jamii. Inapaswa izingatie ubinadamu na kujibu swali, kwa nani tunajali?
6. Inabidi iwe na mchanganyiko wa maandishi, habari picha na vielelezo vyote ambavyo vitamfanya mtu aelewe dhumuni la ujumbe na achukue hatua kutokana na Ushahidi wa takwimu zilizotolewa.

Washiriki wawasilishe kazi zao kabla ya tarehe 13 Novemba 2020, saa kumi jioni.

Kupitia barua pepe ifuatayo:takwimutanzania@gmail.com, Kwa maelezo zaidi wasiliana na Mr. Said Ameir (0784007266), William Matee (0716621067).

limetolewa na Mtakwimu Mkuu wa Serikali;

Ofisi ya Taifa ya Takwimu;

S.L.P 2683;

Dodoma;

Barabara ya Jakaya Kikwete.

**FOMU YA USAJILI KUSHIRIKI SHINDANO LA MWANDISHI BORA WA
HABARI ZA KITAKWIMU**

Jina Kamili:

Taasisi/Chombo cha Habari:

S.L P:

Simu ya Ofisi:

Baruapepe ya Ofisi:

Jina la Mhariri/Mkuu wa Chumba cha Habari:

Anuani yako Binafsi:

Mahala unapoishi:

Mtaa:

Wilaya:

Mkoa:

Simu Binafsi:

Baruapepe Binafsi:

Kichwa cha Habari ya Stori/Makala yako:

Chombo cha Habari kilichochapisha stori/Makala yako:

Toleo na Tarehe iliyochapishwa: